
COVID-19
PWF World Missions Commission
Mapendekezo ya Makanisa
Pentecostal
WORLD FELLOWSHIP
WMC
PENTECOSTAL WORLD
FELLOWSHIP

# PWF TUME YA ULIMWENGU YA UTUME

# MAPENDEKEZO KWA MAKANISA KATIKA KUKABILIANA NA JANGA LA COVID-19

Lengo la kabrasha hii ni kusaidia makanisa kutambua, kupanga, kubadilika na kukabiliana na janga la Corona (Covid-19) kwa sasa. Kurasa zifuatazo zinataarifa kuhusu Corona (Covid-19) ni nini, kwanini makanisa yanapaswa kuitikia katika suala hili tandavu ulimwenguni na imependekeza mbinu za kufanya hivyo. Kwa kuongezea inashauriwa kufuata maagizo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), wataalamu wa afya na serikali yako husika. Kabrasha hii imelenga kupokelewa kama sehemu ya taarifa ya nyongeza kwa mipango ya kitaifa na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) na sio mbadala wake. Imeandaliwa kwa ushirikiano wa taasisi mbalimbali za msaada na maendeleo za Kipentekoste pamoja na wataalamu wa afya. Sehemu kubwa ya yaliyomo yametokana na mapendekezo ya Living Waters (Houston, U.S.) na Tearfund, kati ya wengine wengi. Yaliyomo katika kabrasha hii yanaweza kuboreshwa kulingana na muktadha tofauti na kutafsiriwa kwenye lugha mbalimbali.

Pentecostal WORLD FELLOWSHIP

W M C PENTECOSTAL WORLD FELLOWSHIP

## COVID-19 NI NINI (VIRUSI VYA CORONA)?



**COVID-19**, ina maana ni virusi vya ugonjwa wa corona 2019, ni ugonjwa unoambukiza unaosababishwa na kirusi kipya kilichogundulika kwa jina la corona. Iliainishwa na shirika la afya Duniani (WHO) kuwa ni ugonjwa tandavu (pandemic)mnamo 10/03/2020, kuashiria athari inayoweza kuharibu ulimwengu wote. Inaambukiza sana na kwasasa hakuna chanjo wala tiba. Watu wengi (takribani 80%) hupona kutokana na ugonjwa huu bila kuhitaji uangalizi maalum. Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), takribani mtu mmoja kati ya watu sita wanaopata COVID-19 huwa mgonjwa sana na kupata shida katika upumuaji. Ugonjwa huu ni hatari sana kwa watu wazee na wale waliokuwa kwenye hali ya matibabu awali kama vile shinikizo la damu (presha), matatizo ya moyo au kisukari. Dalili kuu za kawaida za COVID-19 ni homa, hali ya uchovu, kikohozi kisichokoma na kupata shida katika upumuaji; pamoja na hayo,watu wanaweza kutembea na kusambaza COVID-19 bila kuonesha dalili zozote. Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), COVID-19 inaweza kuenea kutoka kwa mtu kwenda kwa mtu kupitia vitone vidogodogo vya maji kutoka puani au mdomoni, vinavyotoka wakati mtu mwenye maambukizi akikohoa au kupiga chafya. Watu wengine huwa kwenye uwezo wa kuambikizwa kwa kugusa sehemu au vitu vilivyo athirika kasha kugusa macho, pua au midomo yao.

## HATUA ZA MSINGI ZA KINGA DHIDI YA COVID-19

Njia bora ya kuzuia kusambaa kwa COVID-19 ni kwa kufuata njia hizi za kinga:



1. Osha mikono yako kila wakati na kwa usahihi kwa maji na sabuni walau kwa sekunde 20. Ikitokea hakuna sabuni na maji, tumia kitakasa mikono (sanitizer) yenye asilimia 60% ya kilevi.
2. Funika mdomo na pua yako kwa mkunjo wa kiwiko chako au karatasi ya tishu unapokohoa au unapopiga chafya; tupa tishu mara moja na osha mikono yako.
3. Epuka kugusa macho yako, pua na mdomo.
4. Epuka mgusano kimwili, ikiwezekana, kaa nyumbani na mbali na mikusanyiko ya watu.
5. Zingatia walau umbali wa mita 1 (futi 3) toka kwa mtu anayekohoa au kupiga chafya.
6. Kaa nyumbani haswa ikiwa unajisikia vibaya. Kama una homa, kikohozi au ugumu katika upumuaji, tafuta utabibu kulingana na miongozo ya afya ya kitaifa.
7. Tumia njia mbadala za kusalimiana ambayo haihusishi mgusano wa mwili.
8. Uwe unafahamu na kufuata ushauri unaotolewa na serikali yako, maafisa wa serikali na watoa huduma ya afya.





## KWANINI MAKANISA YANAPASWA KUKABILIANA NA COVID-19?

Makanisa na wachungaji kwa namna ya pekee wapo kusaidia kupunguza kuenea kwa ugonjwa huu. Mfano ni jukumu muhimu ambalo makanisa na viongozi wa dini walifanya wakati wa janga la Ebola barani Africa.
COVID-19 huenea kwa watu walio na mawasiliano ya karibu. Kama mabadiliko hayatafanyika katika ibada za kuabudu na mikusanyiko mingine, makanisa yanaweza kuwa sehemu ya ugonjwa kuzidi kuenea. Hii inaweza kuwaweka washirika katika hatari ya kuambukizwa COVID-19 na zaidi kuhatarisha maisha ya washirika pamoja na wengine katika jamii inayowazunguka.
Huu ni wakati pia wa kutangaza upendo wa Mungu kwa maneno na vitendo.

Makanisa yanaweza kutekeleza misheni ya maombezi tangazo lisiloweza kutengwa na
maonyesho ya injili inayoonekana katika maisha na kazi ya Yesu.
Makanisa yanaweza kuweka tumaini katika kukabiliana na hofu inayohusiana na COVID-19 na kutunza maisha ya kiroho kwa watu, mihemko, kimwili, kijamii, na mahitaji ya usalama kupitia huduma mbalimbali za kanisa.
Makanisa yanaweza kuongeza njia ambayo tayari wanazungumza kwa niaba ya wale waliotengwa, ili kwamba wasizidi kutengwa katika wakati huu wa dharura katika afya ya umma.

## MAKANISA YANAWEZAJE KUKABILI?


Makanisa yanapaswa kuzingatia kukabiliana kwa njia kuu nne:

**1. PUNGUZA KUENEA KWA COVID-19 KANISANI KWAKO**
Wakati kanisa limeaswa kutoacha ibada na ushirika, inapendekezwa namna mpya ya ibada ili kuepuka kuenea kwa COVID-19 kati ya washarika na kwenye jamii. Wachungaji pia wanaweza kutumia uwezo wao kuhamasisha kuwasilisha jumbe zinazoeleweka.

**A. BORESHA NAMNA YA KUABUDU NA USHIRIKA KUFANYIKA**
Wakati ambapo utunzaji wa masuala ya kiroho na kijamii unaotolewa na kanisa ni muhimu zaidi wakati linapotokea ulimwengu janga kama hili, upendo wetu na kujali mtu kwa ujumla inamaana kwamba tunapaswa pia kuchukua hatua kutunza ustawi wa mwili wa washirika wa kanisa letu na jamii. Ili kuhakikisha kanisa halishiriki katika kuenea kwa COVID-19, inahimizwa kufikiria sana kusimamisha mikusanyiko ya kawaida ya kanisa mpaka hapo tishio la kusambaa kwa ugonjwa litakapoisha. Hii inamaanisha kuwa wabunifu ni namna gani kanisa litaabudu na kuwa na ushirika.

Serikali nyingi tayari, au hivi karibuni, zinazuia mikusanyiko ya umma ikiwemo huduma za ibada. Kwa kuendana na hili, makanisa yanapaswa pia kuzingatia kujiepusha na mkusanyiko au kwa kiwango cha chini wanapaswa kuboresha huduma za kanisa ili kupunguza kuenea kwa COVID-19.

***Kuwa mwenye busara*** *kwa kuwa na taarifa.*
***Kuwa salama*** *kwa kuchukua tahadhari.*
***Kuwa mkarimu*** *kwa kusaidia wengine.*
***Sali****.*



**Mapendekezo ya namna ya kupunguza keanea:**

» Kukutana katika vikundi vidogo chini ya watu 10.
» Waombe watu wenye dalili za maambukizi kuacha kuhudhuria mkutano au ibada.
» Hakikisha watu walio katika makundi hatarishi wasihudhurie huduma za ibada, badala yake wapigiwe simu au uangalizi mwingine.
» Mwambie kila mtu akae au asimame walau mita 1 toka kwa mwingine.
» Kutaneni nje kwenye hewa ya kutosha.
» Epuka mgusano wa mwili ikiwemo kusalimiana. Angalia salamu mbadala iliyotolewa na maafisa afya wa serikali inayoendana na muktadha wa mila zenu.
» Epuka kushirikiana vifaa vya kukomunika kama vikombe na sahani na vikapu vya sadaka.
» Rekodi jumbe za kutuma kupitia mitandao ya kijamii pindi utakaposhindwa kukutana kama ilivyo kawaida.

Kwa kuongezea, hakikisha mara kwa mara unasafisha na kutakasa vyombo na vifaa vya kanisani, hususan maeneo yanayoguswa mara kwa mara, ikiwemo juu, mishikio/vitasa, lecterns na vipaza sauti.

Mwisho, hakikisha kuna vifaa vya kusafishia mikono, ikiwemo sehemu za ziada za kunawa mikono mahali pa kuingilia kanisani.



## B. WASILISHA UJUMBE WA KWELI NA UNAOELEWEKA

Wachungaji wanaweza kutumia nafasi zao za uhamasishaji kuwasilisha jumbe zifuatazo:

» COVID-19 ni ugonjwa mbaya tuonapaswa kuzuia kuenea kwa wengine.
» Dalili kuu za COVID-19 ni homa, uchovu, kukohoa mfululizo na ugumu katika upumuaji.
» Kama mtu anasikia dalili hizo, inapendekezwa ajitenge na jamii (self quarantine) kwa siku 14 na kufuata taratibu za serikali za afya kwa kutafuta matibabu.
» Hatua za msingi za kujikinga dhidi ya COVID-19 (rejea ukurasa wa kwanza)
» Mtu akipata COVID-19, haimaanishi ana maradhi ya kiroho au anaadhibiwa na Mungu.
» Hakuna mtu anayepaswa kunyanyapaliwa kwa kuambukizwa COVID-19 au kulaumiwa kuwa na imani ndogo.
» Watie moyo wale wanaoumwa sana kupata matibabu kulingana na miongozo ya afya kitaifa (angalia mfano uliofanywa na Yesu Luka 17:14).
» Hakuna mtu anayepaswa kulaumiwa kwa kuwa mwangalifu, kubaki nyumbani au kuepuka salamu za kugusana. Badala yake, tabia hiyo ya mfano inapaswa kusisitizwa kanisani.
» Umuhimu wa kuomba kwa ajili ya walioathirika; kuwafariji na kuwatia moyo wale wenye hofu na wasiwasi.

Ujumbe huu unaweza kutolewa kwa njia kama za mahubiri ya mtandaoni (online), rekodi, simu, jumbe fupi za maandishi (sms), mitandao ya kijamii na vyombo vya habari (redio na televisheni).

Zaidi ya hayo, habari nyingi za uongo zinazunguka kuhusu COVID-19. Ni muhimu kwa makanisa na viongozi wa makanisa kushirikisha habari zenye uthibitisho kutoka katika vyanzo vya kuaminika tu.

*Zingatia: Kila wakati rejea zinavyosema mamlaka za nchi na Shirika la Afya Duniani (WHO) inakusisitiza kuwasiliana.*

## C. TOA MFANO WA NJIA SAHIHI ZA KUISHI

Viongozi wa kanisa wanapaswa kuonesha tabia zenye uwezo wa kuokoa maisha:
» Chukua tahadhari zote za kujikinga dhidi ya COVID-19 (rejea ukurasa wa kwanza).
» Kama ukiambiwa kuombea washirika wenye dalili za COVID-19, wakati wa kufanya hivyo zingatia umbali stahiki wa mita 1 (futi 3) na kufuata hatua za kujikinga kiafya.
» Onesha mtazamo mzuri, hatua za dhati na imani kwa Mungu juu ya janga hili.



## 2. UTUNZAJI WA WASHIRIKA WAKO

### A. ANDAA WASHIRIKA KWA WAKATI WA KUTENGWA

Wakati wa mlipuko wa COVID-19, au wakati wa kujaribu kuuzuia, washirika wanaweza kutengana, kuwa na hofu au woga. Watakosa sehemu kuu ya maisha ya kanisani, ambayo ni ushirika na kuabudu na kuomba. Andaa washirika kwa kujitenga kwa kutafuta namna waamini kuwa na mawasiliano na kutoa huduma za kiroho kwa kila mmoja.

Saidia familia kukuza maisha yao ya sala, kusoma biblia, kutafakari na nidhamu zingine za kiroho.

### B. ANDAA NJIA ZA KUWA NA MAWASILIANO NA WASHIRIKA WAKO KUTOA HUDUMA

Hakikisha unamawasiliano ya washarika wako wote (iwezekanavyo) ili kuweza kuwasiliana kupitia mazungumzo ya simu au jumbe fupi za maandishi (sms) wakati wa kutengwa. Unaweza pia kuandaa orodha ya watu waliopo kwenye hatari zaidi (wagonjwa au wazee), kati ya washirika, na hakikisha wana chakula, maji, sabuni na mahitaji mengine ya msingi. Wakati wa kutoa huduma, hakikisha huwaweki hatarini wazee na wale walio na hali fulani kiafya ya kuambukizwa COVID-19.

### C. JIBU WASHIRIKA WAKO KWA MASWALI YA 'KIROHO NA KITHEOLOJIA'

Wakati wa majanga na mateso watu huuliza vitu kama, "Kwanini Mungu anayetupenda anaruhusu tuteseke?". Hii inabaki kuwa swali gumu sana kila wakati na kila sehemu. Ni vizuri kuzungumzia maswali magumu kwa kutafuta busara kutoka kwenye Biblia na maisha ya Yesu. Yesu anaelewa mateso yetu na anaambatana nasi katika hayo, aliteseka kuliko binadamu mwingine yeyote. Yesu pia anafahamu hofu zetu na anatuambia tumtwike Yeye katika maombi (1 Petro5:7). Jukumu la Wakristo katika kipindi hiki cha majaribu inabaki kuwa ni kuleta uponyaji katika ulimwengu ulioharibika, kudhihirisha upendo wa Mungu na utukufu, na kuelekeza watu kwenye utimilifu wa maisha (Yohana10:10) hii ni zaidi ya afya ya mwili.






## 3. HAMASISHA KANISA KUTUNZA JAMII

Kanisa halipo kwa ajili yake yenyewe, bali kumpenda Mungu na kumpenda jirani yetu. Wakristo wanapaswa kushuhudia katika kipindi cha janga hili kwa kuzungumza na kuishi maisha ya matumaini na upendo. Makanisa mengi yana taasisi za kijamii ambazo zinaweza kuzungumzia janga hili kwa njia nyingi kuonesha upendo kwenye jamii zao. Kama kanisa lako tayari lina kikundi cha uhamasishaji au kikundi cha watu waliojitolea, baada ya kujifunza na kutambua njia za msingi za kujikinga dhidi ya COVID-19, angalia namna wanavyoweza kusaidia jamii.

**Mifano ni pamoja na:**

» Shirikiana kwa upana zaidi na mamlaka, asasi za kiraia, makanisa mengine na viongozi wa kiimani.

» Hakikisha jamii nzima inapokea taarifa kuhusu COVID-19 na njia za kujikinga.

» Upatikanaji wa habari kwa wale walio katika mazingira magumu uangaliwe kwa uangalifu wa hali ya juu. Watoto, watu wasiojua kusoma na kuandika, watu wenye ulemavu pia wanahitaji kupata taarifa za namna ya kujikinga pia. Habari zinazofikika zinaweza kuwa kwa kupitia mabango, video, picha rahisi za kuelekeza, video zenye lugha za alama, au vifaa vya kuandikia kwenye mashine za breila.

» Hakikisha jamii nzima ina vifaa vya kuosha mikono na maji.

» Angalia watu waliomo katika mazingira hatarishi na waliotengwa wawe na vyakula vya kutosha na mahitaji mengine ya msingi.

» Shughulikia upweke na hofu kwa kuweka mazungumzo wa mtandaoni au kikundi cha kusaidiana.

» Kama unatumia mitandao ya kijamii kuwa pamoja kama kanisa, hakikisha unawapata wengine katika jamii kupitia mkondo huo huo. Jumbe nzuri za matumaini hufanya kujitenga kuwa ngumu kidogo. Ujumbe mzuri wa matumaini unaweza kufanya jambo la kutengwa kutokuwa gumu san. Kwa njia hii, unawafanya watu kutambua kwamba hawapo peke yao na hofu zao.

» Toa chakula na vifaa kwa wahudumu wa afya ambao wataweza kuzidiwa na mzigo wakati huu wa mlipuko.

» Shirikiana na maafisa wa afya kuweza kutambua kesi za COVID-19 kwenye jamii.

» Shirikisha hadithi kutoka kwenye Biblia na jadili kufahamu zinamaanisha nini kwenye muktadha na wakati huu. Mfano mzuri ni hadithi ya Yesu akituliza dhoruba kwenye kitabu cha **Marko 4:35-41**.

Washarika wanahimizwa kila wakati kushiriki upendo wa Mungu, kwa maneno na vitendo. Wakati huo huo, wakati wa majanga, ni muhimu kutotumia hofu za watu au mategemeo ya msaada kwa madhumuni ya kuinjilisha. Badala yake, zingatia namna gani utawapenda watu zaidi kwa kuwaambia hadithi za jinsi imani yako kwa Mungu inakusaidia kukabiliana na janga hili.

**4. SALA NA MOMBEZI**

Kanisa linaamini kwamba Mungu yupo anashughulika kwa masuala ya binadamu, hivyo ni vizuri kujikumbusha na kuwakumbusha wengine kanisani kwako kwamba tunahitaji kusali na kuomba ili janga la COVID-19 ifike mwisho. Ifuatayo ni sala inayoweza kusaliwa.



***"Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."***
*Philippians 4:6-7*

**MUUNGANIKO WA ULIMWENGU WA KIKRISTO KUPITIA SALA**

Pia, tafadhali fikiria kuhusu kujiunga na harakati za maombi za **Unite 714**, ambayo ina msingi Mungu alitoa kukabiliana na tauni katika kitabu cha 2 Mambo ya Nyakati 7:14. Unaweza kujiunga kushiriki, kupata taarifa zaidi na kwenda na wakati kupitia www.unite714.com. Kila wiki, tutasali sala moja katika makanisa yetu na taasisi zetu ku-hamasisha watu kusali sala hii kila siku saa 1:14 asubuhi na saa1:14 usiku kulingana na wakati katika ukanda wao. Pindi utakapojisajili, utapokea sala ya wiki na lengo la sala ili kuwashirikisha watu wako. Inaweza pia kupatikana kwenye www.pwfellowship.org.

## RASILIMALI NA VIUNGO KADHAA

**» Ujumbe kutoka kwa Dr. Billy Wilson, mwenyekiti wa PWF na Empower 21**
https://vimeo.com/399229556

**» Ujumbe kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**
https://www.facebook.com/watch/?v=911052209328888

**» Shirika la Afya Duniani**

https://www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019
https://www.who.int/news-room/q-a-detail/q-a-coronaviruses
https://www.facebook.com/WHO/videos/vb.154163327962392/513817142873722/?type=2&theaterWhat's App WHO Health Alert Group

**»Baraza la Makanisa Ulimwenguni**
https://www.oikoumene.org/en/resources/documents/covid-19

***SALA YA ULIMWENGU***

*Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja mbele ya kiti chako cha enzi cha upendo na neema kupitia mwanao mpendwa, Mkombozi wetu Yesu Kristo. Tunakuja na maarifa ya kufariji uliyotuambia, "Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana na mambo yenu" (1Petro5:7). Tunashukuru unafahamu fadhaa zetu na shida zetu. Tunashukuru kwa hekima yako ya Kimungu ambayo unatukirimia wote tukuombao. (Yakobo1:5).*

*Tunapoomba kwaajili ya watu wote duniani, tunaomba ya kuwa Roho wako Mtakatifu atuoneshe Huruma yako, Ukweli Wako, Rehema yako, Mapenzi yako na kwamba hakuna atakayepotea. Kupitia neno lako na Roho wako, tuongoze katika toba kibinafsi na kwa makundi. Ufalme wako na mapenzi yako yatimizwe duniani kama huko mbinguni.*

*Tunapoomba kwaajili ya wale wanaoteseka kutokana na madhara ya COVID-19; wale wanaoumwa majumbani, wagonjwa waliopo mahospitalini na vituo vya afya, wale wanaowauguza wapendwa wao wagonjwa. Tunaomba damu ya Yesu kuleta neema ya uponyaji.*

*Tunawaombea maskini, walio katika hali ngumu na wanaohangaika kupata huduma stahiki za afya. Bwana wahurumie. Mioyo yetu iwaangalie na tuwageukie kushughulika na mahitaji yao.*

*Tunawoambea wanaume kwa wanawake wanaotoa huduma katika nafasi mbali mbali za afya. Tunashukuru kwa utayari wao kuhatarisha maisha yao wenyewe. Walinde wao na familia zao.*

*Baba yetu wa Mbinguni, asante kwasababu tunakuja mbele zako na kamwe husinzii wala haulali. Hata uonavyo shomoro na nywele zetu kichwani, unajua hali zetu za kusikitisha. Njoo Roho Mtakatifu, tuletee matumaini, tuletee faraja, tuletee amani na upendo kwako na kwa kila mmoja wetu. Kwa Jina la Baba , na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amen.*

***Na Dr. A.D. Beacham***
*Katibu, Ushiriki Wa Kipentekoste Ulimwenguni*
*Msimamizi Mkuu,IPHC*

Pentecostal WORLD FELLOWSHIP

W M C PENTECOSTAL WORLD FELLOWSHIP